



HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini



Shree Tanzania Swamirayan Mandir yatoa Misaada Chalinze

Taasisi ya Shree Tanzania Swaminarayan Mandir watoa misaada mbalimbali kwa wazee na Wanafunzi Chalinze

Taasisi ya dini ya kihindi ijulikanayo kama Shree Tanzania Swaminarayan Mandir yenyе makao makuu jijini Dar es Salaam imetoa msaada wa vyakula kwa wazee wapatao 200 na kutoa vifaa vya kujifunzia(Madaftari na Kalamu) kwa wanafunzi zaidi ya 1000 katika Kata ya Msoga,Halmashauri ya wilaya ya Chalinze.

Wanafunzi wapatiwa
Madaftari na kalamu

Toleo Maalum
18,Januari 2023



Taasisi hiyo imetoa vyakula mbalimbali kama mchele, maharage, sukari na chumvi. Vyakula hivyo vimetolewa leo katika Ofisi ya Kata ya Msoga. Vyakula hivyo vimetolewa na shirika hilo kama utaratibu wa dhehebu hilo kutoa sadaka kwa jamii kila mwaka kama sehemu ya ibaada misaada hii Ni maalum kwa sababu ya msikiti mkuu ulioko India unakamilisha miaka 200 mwaka huu hivyo dhehebu lina kila sababu ya kutoa sadaka kwa kumshukuru Mungu kwa kuliwezesha dhehebu hilo kuendelea kukua. Kwa upande wa vifaa vya kufundishia Taasisi imetoa madaftari na kalamu kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi darasa la tatu wapatao 1074 wanaosoma Shule za Msingi Msoga, Mboga na Lunga, Lubaya na Changa zote za kata ya Msoga.

Wazee Wapatiwa vyakula mbalimbali

Aidha kwa upande wake Diwani wa Kata ya Msoga, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze Mheshimiwa Hassani Mwinyikondo alitoa shukrani zake za dhati kwa Taasisi hiyo kwa moyo wa upendo kwa wananchi wake hususan kwa kundi maalum la wazee kwa kuwapatia vyakula ili kuboresha afya zao. Halikadhalika alitoa shukrani kwa Taasisi hiyo kwa kutoa madaftari na kalamu kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi zaidi ya 1000 katika Kata ya Msoga.



Chalinze District Council



ChalinzeDC onlineTV



chalinze_district_council